

Adhabu

Adelheid Marie Bwire
Kiswahili






Siku moja mamangu alinunua matunda mengi sana.

Mimi na ndugu zangu
tulijiuliza lini mama
angetugawia ili tule.





Baadaye, kakangu,
Rahim, alijificha.

Aliyala matunda yale
yote peke yake!

Mimi na ndugu yangu tulipogundua, tulilia tukisema, “Rahim ni mtukutu tena ni mchoyo.”





Mama alikasirika sana alipogundua kwamba matunda yote yalikuwa yameliwa.


Mimi na ndugu yangu
tulimwalia Rahim
kwa macho makali.





Tulmwuliza mama ikiwa
angemwadhibu Rahim.

Lakini, Rahim alipata
adhabu ambayo
hatukutarajia.





Rahim hakuweza kutulia
pahali pamoja!

Mama alipomwuuliza alijibu kwa sauti ya chini, “Naumwa na tumbo.”





Sote tuliona kwamba hiyo ilikuwa adhabu mbaya kuliko kama Rahim angechapwa na mama.

Baadaye alipopata nafuu, Rahim alituomba msamaha.



Adhabu

Writer: Adelheid Marie Bwire

Illustration: Melany Pietersen

Language: Kiswahili



© African Storybook Initiative and Molteno Institute,
2014



This work is licensed under a Creative Commons Attribution
(CC-BY) Version 3.0 Unported Licence

Disclaimer: You are free to download, copy, translate or adapt this
story and use the illustrations as long as you attribute or credit the
original author/s and illustrator/s.

Saide 
South African Institute
for Distance Education
www.africanstorybook.org
A Saide Initiative